

COVID-19

Afya na usalama wa kazi: Habari kwa wafanyakazi

Chini ya mfano wa sheria za Afya na Usalama wa Kazi, mwajira wako ana jukumu la kutunza afya na usalama wa wafanyakazi wao na wengine kwa mahali pa kazi.

Wafanyakazi wanahitaji kufanya nini?

Una jukumu la kutunza kwa maana afya na usalama wako mwenyewe, na sio kuathiri vibaya afya na usalama wa wengine.

Unahitaji kufuata sera au maelekezo yoyote mwafaka ambayo mwajiri wako ameweka ili kujibu COVID-19. Hii ni pamoja na ikiwa unafanya kazi kutoka eneo lingine, kama vile kufanya kazi nyumbani.

Wajiri wanahitaji kufanya nini?

Mwajiri wako anapaswa kutambua hatari za afya na usalama wa kazi kutokana na kuhatarishwa na virusi vya COVID-19, na inapowezekana, kuweka udhibiti sahihi. Wanahitaji kufuata maagizo ya serikali, pamoja na kutekeleza [kuweka umbali wa kimwili \(physical distancing\)](#) - kuwaweka kila mtu hapo mahali pa kazi angalau umbali wa kimwili mita 1.5.

Hatari kutoka kwa virusi vya COVID-19 inaweza kuwa ya kimwili au ya kisaikolojia.

Kile ambacho mwajiri wako anaweza kufanya ili kusimamia hatari ya kuambukizwa na virusi vya COVID-19 itategemea mahali pako pa kazi na kazi unayofanya. Mwajiri wako anapaswa kuongea na wewe juu ya yale anayepanga kufanya.

Wangeweza:

- kuweka hatua za kuzuia kukaribiana kwa karibu kati ya watu - weka kila mtu wapo mahali pa kazi angalau umbali wa kimwili wa mita 1.5.
- hamisha kila mtu hapo mahali pa kazi kufanya [usafi mzuri \(good hygiene\)](#) kwa kutoa huduma za vituo vya usafi vinavyofaa ili kuwezesha wafanyakazi kuosha mikono yao kwa sabuni na maji kwa angalau sekondi 20, au kutumia sanitaiza inayotokana na pombe
- kutoa upatikanaji wa vifaa vya kinga binafsi
- kuongeza kusafisha katika mahali pa kazi
- kupunguza upatikanaji wa mahali pa kazi na watu wengine
- kukuelekeza kufanya kazi kwa eneo lingine, kama vile nyumba yako - kumbuka hii inaweza kubadilika, kuongezeka au kuunda hatari za kiafya na usalama za kazi

Je! Nifanye nini kama nafikiri nina COVID-19?

Unapaswa:

- [kutpata ushauri wa matibabu \(seek medical advice\)](#)
- usiende kazini

- kumwambie mwajiri wako haraka iwezekanavyo na umsisishe ikiwa hali yako itabadilika, kwa mfano ikiwa umethibitishwa kuwa unavyo virusi

Je! Naweza kuacha kazi ikiwa sio usalama?

Ikiwa una wasiwasi juu ya usalama wako, zungumza na mwajiri wako au Mwakilishi wa Afya na Usalama (HSR).

Katika hali zingine wafanyakazi wana haki ya kuacha au kukataa kufanya kazi isiyo salama. Una haki hii ikiwa kuna wasiwasi inayofaa kuwa unaweza kuonyeshwa kwa hatari kubwa kwa afya na usalama wako kutoka kwa hatari ya mara moja au inayowezekana - hii inaweza kuwa pamoja na kuhatarisha kwa virusi vya COVID-19.

Ikiwa utaacha kazi kwa sababu sio salama, unahitaji kumwambia mwajiri wako haraka iwezekanavyo. Unapaswa pia kuwepo ili kufanya kazi mbadala inayofaa, kama vile kufanya kazi kutoka nyumbani.

Habari zaidi

Kwa habari juu ya afya na usalama wa kazi, nenda kwenye [tovuti ya Safe Work Australia \(Safe Work Australia website\)](#)

Kwa habari juu ya likizo yako na malipo, nenda kwa [Mchunguzi Mkuu Haki ya Kazi \(Fair Work Ombudsman\)](#)

Kwa habari ya afya, nenda kwa health.gov.au

Tafadhali kumbuka mfano wa sheria za WHS zimetokelezwa katika mamlaka zote isipokuwa Viktoria na Australia Magharibi. Kwa habari maalum juu ya eneo lako la kazi, tafadhali wasiliana na [mdhibiti anayehusika wa WHS katika jimbo au wilaya yako \(WHS regulator in your state or territory\)](#).